# CHUO CHA SANAA DAR ES SALAAM

*"Kipaji ni Ajira. Sanaa ni Biashara"*

## MAELEKEZO YA KUJIUNGA KWA MWAKA WA MASOMO 2025/2026

### 1. KUHUSU CHUO CHA SANAA DAR ES SALAAM

**Chuo cha Sanaa Dar es Salaam** ni Chuo cha kisasa kinachoongoza nchini Tanzania kwa kutoa mafunzo ya Sanaa za aina nyingi za Kitamaduni na za Kisasa, yanayojikita zaidi kwenye mazoezi ya vitendo yanayohakikisha kila mwanachuo bila ya kujali tofauti zake za umri, hali, nafasi, kipato, elimu na uelewa, anakuwa mahiri.

Wakati wa mchakato wa kusajiliwa, wanachuo wanahudhuria Kliniki ya kuibua vipaji vya Sanaa ili kubaini vipaji na viwango vya umahiri walivyonavyo. Chuo pia kinafundisha lugha ya Kiswahili kwa wageni na kinawafundisha wanachuo wake Kiingereza na Kichina.

Kusoma **Chuo cha Sanaa Dar es Salaam** ni zaidi ya kujifunza; kwani Chuo kinaibua, kukuza na kuendeleza vipaji kuwa ujuzi wa kitaalamu. Pia huwasaidia wahitimu kujiajiri au kuajiriwa kupitia vipaji vyao. Pamoja na Mafunzo ya Darasani wanachuo hupata Mafunzo ya Uanagenzi, pia wanasaidiwa kubadilisha Sanaa zao kuwa biashara rasmi na kumudu kuzisimamia au kusimamia wasanii wengine. Maisha Chuoni ni aina fulani ya burudani, kwani wanachuo husoma huku wakijiongezea kipato kupitia Sanaa wanazotayarisha wenyewe pamoja na kupata fursa ya kuonesha Sanaa zao kwenye matamasha mbalimbali pamoja na vituo vya TV. Chuo kinawaunganisha (*connection*) wanachuo na wasanii maarufu na taasisi zinazojishughulisha na Sanaa.

Hapa Chuoni ndoto ya kila mwanachuo inaheshimiwa na kuwekewa mikakati mahsusi ya kuhakikisha kila mwanachuo mbali ya kufundishwa, anasaidiwa kutimiza ndoto yake katika Sanaa.

Chuo kina Usajili Kamili kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (**NACTVET**) kwa namba **REG/NACTVET/1125**. Na kimeidhinishwa na Baraza la Sanaa la Taifa (**BASATA**), Bodi ya Filamu Tanzania (**TFB**) na Baraza la Kiswahili la Taifa (**BAKITA**).

### 2. MAHALI CHUO KILIPO

Chuo kipo mkono wa kulia kama unatoka Kituo cha Mabasi cha Magufuli/Mbezi Luis kuelekea Kibaha, kando ya barabara ya Morogoro katika mtaa wa Kibamba, Dar es Salaam, Tanzania.

### 3. KOZI ZINAZOTOLEWA

#### 3.1. Kozi Ndefu:

a. Sanaa za Maonesho na Ubunifu *(Performing Art and Design)*
b. Uzalishaji wa Filamu na Vipindi vya TV *(Film and TV Production)*
c. Ubunifu wa Muziki na Sauti *(Music and Sound Design)*

#### 3.2. Kozi Fupi:

a. Sanaa za Kazi za Mikono na Dijitali; Utaalamu wa **Uchoraji na Mapambo**
b. Sanaa za Kazi za Mikono na Dijitali; Utaalamu wa **Ubunifu wa Picha na Michoro (Graphic Design)**
c. Sanaa za Kazi za Mikono na Dijitali; Utaalamu wa **Ubunifu wa Picha/Michoro Jongefu (Animation Design)**
d. Sanaa za Kazi za Mikono na Dijitali; Utaalamu wa **Uchongaji Vinyago**
e. Sanaa za Kazi za Mikono na Dijitali; Utaalamu wa **Ususi wa Vifaa vya Kitamaduni**
f. Sanaa ya Urembo; Utaalamu wa **Urembo wa Nywele**
g. Sanaa ya Urembo; Utaalamu wa **Makeup**

h. Sanaa ya Urembo; Utaalamu wa **Utunzaji Ngozi**
i. Sanaa ya Urembo; Utaalamu wa **Utunzaji Kucha (Nail Care), Matibabu ya Mikono (Manicure), na Matibabu ya Miguu (Pedicure)**
j. Sanaa ya Urembo; Utaalamu wa **Mapambo**
k. Ubunifu wa Mitindo na Mavazi ya Vionjo; Utaalamu wa **Ubunifu wa Mitindo (Fashion Design)**
l. Ubunifu wa Mitindo na Mavazi ya Vionjo; Utaalamu wa **Mitindo ya Mavazi ya Vionjo (Costume Design)**
m. Ubunifu wa Mitindo na Mavazi ya Vionjo; Utaalamu wa **Uanamitindo**
n. Muziki na Ngoma; Utaalamu wa **Kuimba Muziki (Bongo Fleva)**
o. Muziki na Ngoma; Utaalamu wa **Alama za Muziki (Musical Notation)**
p. Muziki na Ngoma; Utaalamu wa **Sauti ya Kuimba (Vocal)**
q. Muziki na Ngoma; Utaalamu wa **Upigaji wa Ala za Muziki**
r. Muziki na Ngoma; Utaalamu wa **Uchezaji wa Muziki (kudance na keorografia)**
s. Muziki na Ngoma; Utaalamu wa **Ngoma za Asili**
t. Ubunifu wa Sauti na Muziki; Utaalamu wa **Ubunifu wa Sauti (Sound Design)**
u. Ubunifu wa Sauti na Muziki; Utaalamu wa **Uzalishaji wa Muziki (Music Production)**
v. Uigizaji kwa ajili ya Jukwaani na Filamu; Utaalamu wa **Uigizaji wa Hadharani**
w. Uigizaji kwa ajili ya Jukwaani na Filamu; Utaalamu wa **Uigizaji wa Filamu, na Video za Muziki**
x. Uigizaji kwa ajili ya Jukwaani na Filamu; Utaalamu wa **Uigizaji Sauti**
y. Uigizaji kwa ajili ya Jukwaani na Filamu; Utaalamu wa **Utambaji wa Hadithi na Masimulizi**
z. Uzalishaji wa Filamu na Vipindi vya TV; Utaalamu wa **Uongozaji wa Video (Video Directing)**
aa. Uzalishaji wa Filamu na Vipindi vya TV; Utaalamu wa **Uzalishaji wa Filamu na Vipindi vya TV**
ab. **Mahitaji Mahsusi (Tailor-made)***
ac. **Usimamizi wa Sanaa (Art Management)**
ad. **Lugha ya Kiswahili kwa wageni**

**Kozi za Mahitaji Mahususi ni kozi maalum zinazoundwa ili kukidhi mahitaji na matakwa maalum ya wanafunzi binafsi au vikundi/taasisi. Kozi hizi hubinafsishwa ili kushughulikia ujuzi maalum, maarifa, au ustadi ambao wanafunzi wanahitaji kujipatia, kulingana na malengo yao binafsi au ya kitaaluma.*

## 4. SIFA ZA KUJIUNGA

a. Kozi ndefu zote na Kozi fupi ya Usimamizi wa Sanaa *(Art Management)*, awe na elimu ya angalau Kidato cha Nne *(Form IV)*.
b. Kozi fupi zote, ajue kusoma na kuandika.
c. Kozi za Mahitaji Mahsusi, awe na uzoefu katika Sanaa na kujua kusoma na kuandika.

## 5. MUDA WA KUPOKEA WANACHUO

Wanachuo wanapokelewa muda wowote wa mwaka.

## 6. MUDA WA KUANZA MASOMO *(INTAKES)*

a. Kozi ndefu masomo yanaanza katika miezi ya Machi na Oktoba.
b. Kozi fupi masomo yanaanza katika miezi ya Februari, Mei, Agosti na Novemba ya kila mwaka.
c. Kozi za Mahitaji Mahsusi na Kozi ya Lugha ya Kiswahili kwa Wageni, masomo huanza muda wowote kwa makubaliano na Mwombaji.

## 7. MUDA WA KUSOMA

a. Kozi ndefu zinasomwa kwa miezi kumi na miwili (12).
b. Kozi fupi zinasomwa kwa miezi mitatu (3). Kozi fupi zimepangwa kwa hatua tatu ambazo ni Hatua ya Awali *(Basic Level)*, Hatua ya Kati *(Intermediate Level)* na Hatua ya Juu *(Advanced Level)*. Baada ya kuhudhuria Kliniki ya Kuibua Vipaji, mwanachuo atachagua hatua inayomstahili kusajiliwa.
c. Kozi za Mahitaji Mahsusi na Lugha ya Kiswahili kwa Wageni hazina muda maalum kutegemea na uhitaji na nafasi ya Mwanachuo. Hata hivyo, muda wa juu wa Kozi za Mahitaji Mahsusi ni siku thelathini (30) na Kozi ya Lugha ya Kiswahili kwa Wageni ni siku sitini (60). Kozi ya Lugha ya Kiswahili kwa Wageni imepangwa kwa hatua tatu kila moja inayojitegemea, ambazo ni Hatua ya Awali *(Beginners Level)*, Hatua ya Kati *(Intermediate Level)* na Hatua ya Juu *(Advanced Level)*.
d. Usomaji kwenye Zamu za Muda Mfupi na Madarasa ya Nyumbani hurefusha muda wa kusoma.

## 8. ZAMU ZA KUSOMA

Kuna zamu tofauti za aina nne kwa siku, ambazo ni **Zamu ya Asubuhi**, **Zamu ya Jioni, Zamu ya Muda Mfupi** *(part-time shift)* na **Madarasa ya Nyumbani** kutegemea na uchaguzi wa Mwombaji. Kwa kozi moja, mwanachuo anapaswa kuhudhuria zamu moja tu kwa siku. Zamu ya Asubuhi inaanza saa 1:30 asubuhi hadi saa 10:00 jioni, na Zamu ya Jioni inaanza saa 11:00 jioni hadi saa 3:00 usiku, kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa. Jumamosi kunakuwa na zamu moja kwa wanachuo wote, kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri. Katika Zamu ya Muda Mfupi, Mwanachuo hujichagulia siku na muda anaotaka kufika na kutoka Chuoni kulingana na nafasi yake. Kwa upande wa Madarasa ya Nyumbani, Mwanachuo hujichagulia mahali pa kusomea na muda anaotaka kuanza na kumaliza masomo kwa siku kulingana na nafasi yake. Hatufanyi kazi siku za Jumapili na siku za mapumziko ya Kitaifa.

**Zingatia:**

- *Madarasa ya Nyumbani ni kwa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani* pekee.*
- *Kusoma kwenye Zamu ya Muda Mfupi na Madarasa ya Nyumbani kunaweza kuongeza gharama.*

## 9. KUSOMA KOZI ZAIDI YA MOJA KWA WAKATI MMOJA

Inaruhusiwa mwanachuo kusoma kozi zaidi ya moja kwa wakati mmoja. Kila kozi atasajiliwa tofauti na atapaswa kulipia gharama zote zinazohusika kwa kila kozi. Na usomaji utakuwa kwenye zamu tofauti kwa siku.

## 10. UTARATIBU WA UVAAJI NGUO CHUONI

Wanachuo wanaruhusiwa kuvaa Chuoni viatu au nguo zozote wazipendazo. Hata hivyo, **nguo zinazoonesha sehemu yoyote ya mwili kutoka kifuani hadi magotini pamoja na kwapa au zinazoonesha nguo za ndani haziruhusiwi kuvaliwa Chuoni**. Chuo kina utaratibu wa kushiriki kwenye sherehe na shughuli mbalimbali za Chuo, za Kiserikali au za kijamii ambapo wanachuo wanatakiwa kuhudhuria wakiwa wamevaa fulana za Chuo.

## 11. VIPODOZI NA UREMBO

Matumizi ya vipodozi na urembo yanaruhusiwa, ikiwemo kusuka nywele kwa mtindo wowote. Wanachuo wanafundishwa na kuhamasishwa kuwa warembo au watanashati wakati wote ndani na nje ya Chuo.

## 12. GHARAMA ZA HOSTELI

Gharama za hosteli za Chuo ni Tsh. 70,000/= kwa mwezi. Hosteli ina vitanda, magodoro, umeme, maji, malezi na ulinzi. **Kuishi hostel ni hiari**.

## 13. ZANA/VIFAA VYA SANAA KWA MATUMIZI BINAFSI

Wanachuo wanaruhusiwa kuja na zana au vifaa binafsi vya Sanaa wanavyopenda na wanavyomudu kutegemea na kozi wanazokuja kusoma, kwa ajili ya matumizi yao binafsi.

## 14. KUFANYA MAZOEZI YA VITENDO *(PRACTICAL)*

Sehemu kubwa ya mafunzo yetu hutolewa kwa vitendo. Wanachuo huhudhuria sehemu mbalimbali kwa ajili ya Uanagenzi na kujizoeza kwa vitendo; hii ni pamoja na kushiriki kwenye mashindano, sherehe, maonesho na matamasha mbalimbali.

## 15. KUFANYA MAFUNZO YA VITENDO UWANDANI *(FIELD WORK ATTACHMENT)*

a. Wanachuo huhudhuria mafunzo ya vitendo uwandani *(field).*
b. Chuo kwa kushauriana na wanachuo au wazazi/wadhamini, huwatafutia maeneo ya kufanyia *field*.
c. Wanachuo hujigharamia nauli, malazi na chakula kwa ajili ya *field.*

## 16. MATUMIZI YA SIMU ZA MKONONI CHUONI

a. Wanachuo wanaruhusiwa kutumia simu za mkononi wakiwa Chuoni. Chuo kinahimiza matumizi ya simu kwa uwajibikaji na heshima wakati wote.
b. Wanachuo wanafundishwa matumizi bora ya mitandao ya kijamii kwa ajili ya kujiongezea kipato.

## 17. VIWANGO VYA ADA

| S/N | Kozi | Ada (TZS) | Muda |
|---|---|---|---|
| 1. | Kozi ndefu | 800,000 | Mwaka 1 |
| 2. | Kozi Fupi | 500,000 | Miezi 3 |
| 3. | Kozi za Mahitaji Mahsusi | 300,000 | Mwezi 1 |
| 4. | Kozi ya Lugha ya Kiswahili kwa Wageni | 25,000/saa moja | Miezi 2 |

## 18. MICHANGO

| Huduma/Kifaa | Gharama (TZS) |
|---|---|
| Usajili | 25,000 |
| Kitambulisho | 20,000 |
| Fulana | 25,000 |
| Serikali ya wanachuo | 10,000 |
| Ada ya matengenezo *(Madarasa/Studio/Maabara/Saluni)* | 30,000 |
| Usimamizi wa mazoezi na mafunzo ya vitendo uwandani* | 100,000 |

** Kozi za Mahitaji Mahsusi na Lugha ya Kiswahili kwa Wageni hazihusiki na mchango huu.*

## 19. MASUALA YA KUZINGATIA KATIKA ULIPAJI WA ADA NA MICHANGO

a. Malipo ya **Ada ya Maombi** *(rejea Sehemu ya 8.c. ya Fomu ya Maombi)* yafanywe kupitia mfumo wa LIPA KWA SIMU kwenda LIPA NAMBA ya YAS **16348015,** jina **CHUO CHA SANAA DAR ES SALAAM**.

b. Malipo yote yaliyoainishwa katika vifungu vya 17 na 18 vya fomu hii hapo juu yanapaswa kufanywa kwa kutumia **Namba ya Kumbukumbu** *(Control Number).* Wanachuo wanashauriwa kupata Namba ya Kumbukumbu kutoka Chuoni kabla ya kufanya malipo hayo (namba hizo zinatofautiana kwa ajili ya malipo ya ada na michango mingine).

c. Ada inaweza kulipwa kwa mkupuo au kwa awamu kulingana na anavyopata.

d. Chuo hakipokei malipo kwa fedha taslimu. **Katika mazingira yoyote, usikabidhi pesa taslimu au kwa simu kwa mfanyakazi yeyote wa Chuo kwa ajili ya kulipia chochote.**

**e. Malipo yoyote yakifanywa, hayawezi kuhamishwa wala kurejeshwa**.

## 20. BARUA YA KUJIUNGA NA CHUO

Baada ya maombi kushughulikiwa, Mwombaji atajulishwa kwa ujumbe mfupi wa simu kupitia namba yake na ya Mdhamini wake. Iwapo maombi yake yatakubaliwa atatumiwa Barua ya Kujiunga na Chuo.

## 21. FOMU YA UCHUNGUZI WA MATIBABU

Barua ya kujiunga na Chuo itaambatishwa na Fomu ya Uchunguzi wa Matibabu, au Mwombaji anaweza kuipakua fomu hiyo kwenye tovuti ya Chuo www.dararts.ac.tz, ambapo atakwenda nayo kufanya uchunguzi wa matibabu kwenye **hospitali** au **kituo cha afya** kinachotambulika na Serikali.

## 22. NYARAKA ZA KUWASILISHA KWENYE USAJILI

Anapokuja kuripoti Mwombaji anatakiwa aje na picha mbili *(passport size)*, **nakala halisi** za vyeti alivyoambatisha kwenye fomu yake ya maombi *(rejea Sehemu 8.b. ya Fomu ya Maombi)*, **nakala halisi** ya Fomu ya Uchunguzi wa Matibabu iliyojazwa, na **nakala kivuli** ya Barua ya Kujiunga na Chuo.

## 23. ZINGATIA

Chuo kinaongozwa na Sheria, Sheria Ndogo, Kanuni na Taratibu ambazo wanachuo wanapaswa kuzitii.

## 24. KWA MAWASILIANO ZAIDI

Iwapo una hoja usisite kufika Chuoni au kupiga simu kwenye namba **0715 910 010.**